

Maelezo ya Ukweli Kuhusu COVID-19

Namna za kujitambulisha zinazokubalika kwa ajili ya miadi za chanjo

Baada yako [kustahiki kupokea chanjo ya COVID-19](#) katika jimbo la Ohio na [unajiandaa kwa miadi ya kupokea chanjo au ya kliniki](#), hakikisha kwamba umebeba namna ya kujitambulisha inayokubalika.

Mhudumu anayetoa chanjo atahitaji kuthibitisha **utambulisho, jina na umri wako**. Huhitajiki kuwasilisha ithibati ya uraia au hali ya ukazi. Kitambulisho chako kitakubaliwa hata ikiwa muda wake wa matumizi umekwisha au kilitolewa na jimbo au nchi nyingine.

Ikiwa unastahiki kupokea chanjo kwa msingi wa kazi yako (k.m. mfanyakazi wa shule wa madaraja ya K-12 au mhudumu wa afya), Jimbo la Ohio halihitaji hati zozote za ziada ili kuthibitisha ustahiki wako; hata hivyo, wanaotoa chanjo huenda wakaweka taratibu zao za kuchunguza na kufuatilia ili kutathmini ustahiki.

Kabla ya miadi yako, tunakushauri kwamba uwasiliane na wanaokupa chanjo ili kuthibitisha hati utakazohitaji kwa ajili ya miadi yako. Namna za kujitambulisha zinazokubalika zimeorodheshwa hapa chini:

- Leseni ya dereva au kitambulisho chochote chenye picha, bila kujali tarehe ya mwisho wa matumizi chake au eneo kilipotolewa.
- Kitambulisho cha mwanajeshi anayehudumu/alijestaaifu.
- Taarifa kutoka kwa tabibu (ikijumuisha rekodi za chanjo).
- Rekodi za sensa.
- Rekodi za uasili.
- Cheti cha uraia wa kujiandikisha.
- Cheti cha kuzaliwa: Cheti cha kuzaliwa, huku kikiwa hati ya asili au nakala iliyothibitishwa.
- Kitambulisho kilichotolewa na ubalozi wa nchi yako ya asili.
- Pasipoti au kadi ya pasipoti.
- Cheti cha uraia.
- Kadi ya hali ya ukazi wa kudumu.
- Hati ya kuomba kubadilishiwa cheti cha uraia wa kujiandikisha/uraia wa Marekani.
- Fomu kutoka kwa Idara ya Mambo ya Nje ya Marekani.
 - Rekodi za huduma katika jeshi (DD-214)
 - Uthibitisho wa Kuzaliwa kwa Raia wa Marekani Katika Nchi ya Kigeni (FS-545)
 - Uthibitisho wa Ripoti ya Kuzaliwa kwa Raia wa Marekani Katika Nchi ya Kigeni (DS-1350)
 - Ripoti ya Kuzaliwa kwa Raia wa Marekani Katika Nchi ya Kigeni Kutoka kwa Ubalizi (FS-240)
 - Hati ya Kuthibitisha Ajira (I-766/EAD)
 - Hati ya usafiri (I-797F)

Ilibuniwa mnamo Februari 26, 2021.

Kwa maelezo zaidi, tembelea coronavirus.ohio.gov.

Kwa majibu ya maswali yako kuhusu COVID-19, piga simu kwa nambari 1-833-4-ASK-ODH (1-833-427-5634).

Afya ya akili yako ni muhimu sawia na afya ya mwili wako. Ikiwa wewe au mpendwa wako anakabiliwa na wasiwasi unaohusiana na janga la coronavirus, unaweza kupata usaidizi saa 24 kwa siku, siku saba kwa wiki. Piga simu ya huduma za usaidizi wa COVID-19 kupitia 1-800-720-9616.